# CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHA NGOME

## (NGOMESACCOS LTD)

**DSR 991**

## SERA YA UWAKILISHI.

**TOLEO LA I : 2020**

# CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHA NGOME

## (NGOMESACCOS LTD)

**DSR 991**

## SERA YA UWAKILISHI.

**TOLEO LA I : 2020**

**YALIYOMO**

HISTORIA YA CHAMA....................3

UTANGULIZI....................3

UWAKILISHI....................3

UCHAGUZI NA MICHAKATO YAKE....................5

HITIMISHO....................7

# SERA YA UWAKILISHI WA NGOME SACCOS LIMITED

## 1.0 HISTORIA YA CHAMA

NGOME SACCOS LTD yenye nambari ya usajiri DSR 991 ilisajiliwa tarehe 30 April 2007, chini ya sheria ya Ushirika No. 20 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2004, kama inavyorejewa na sheria ya sasa ya Ushirika No. 6 ya mwaka 2013 na kanuni zake za mwaka 2015. Wanachama wa Ngome SACCOS Ltd wanatokana na fungamanisho (common Bond) ya Maafisa ,Maaskari , Wastaafu pamoja na Watumishi wa Umma wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na wale waliohamia wizara nyingine wakiwa wanachama Hai wa Ngome SACCOS.

## 2.0 UTANGULIZI

Kwa mujibu wa kanuni ya vyama vya ushirika ya mwaka 2015, kanuni ya 45. Kanuni inatoa wigo kwa SACCOS zenye wajumbe wengi kutokana na ukubwa wake kuwa na wawakilishi wa wanachama kwenye Mkutano Mkuu. Sera hii inatoa dira ya uwakilishi utakavyokuwa na namna wawakilishi watakavyopatikana.

## 3.0 UWAKILISHI

### 3.1 WAWAKILISHI

Kutakuwa na wawakilishi, idadi yake ikitegemea vikosi vilivyoko katika kila mkoa na maeneo yote ya nchi yatakayohusisha Maafisa, Askari, Watumishi wa umma na wastaafu, watakaopatikana kwa utaratibu wa kuchaguana kwa uchaguzi utakaofanyika kila baada ya miaka mitatu (3)

### 3.2 MGAWANYIKO WA WAWAKILISHI

(a) Idadi ya jumla ya wawakilishi itategemea vikosi vilivyopo, na kila kikosi kitakuwa na wawakilishi wawili kwa uwiano wa Maafisa, Askari na Watumishi wa umma isipokuwa pale ambapo hakuna uwiano huo.

(b) Idadi ya Wastaafu itakuwa kumi na nane (18), wawili kila kanda kulingana na kanda zilizopo;

(i) Kanda ya Kaskazini
(ii) Kanda ya Ziwa
(iii) Kanda ya Kati
(iv) Kanda ya Magharibi
(v) Kanda ya Mashariki
(vi) Kanda ya Nyanda za juu Kusini
(vii) Kanda ya Zanzibar (Pemba mmoja na Unguja mmoja)
(viii) Kanda ya Dar es Salaam na Pwani
(ix) Kanda ya Kusini

## 3.3 SIFA ZA MWAKILISHI

Mwakilishi atakuwa na sifa zifuatazo;

(a) Mwanachama hai (anayetimiza masharti ya chama).
(b) Mwenye ufahamu mzuri wa chama na sheria za ushirika.
(c) Muadilifu.
(d) Anayeshiriki kikamilifu shughuli za chama.
(e) Awe mwanachama kwa muda usiopungua miaka miwili, isipokuwa tu pale ambapo Tawi ni jipya, na wanachama waliopo hawatimizi kigezo hicho.
(f) Awe na elimu ya angalau kidato cha nne.
(g) Awe na uwezo wa kushawishi wanachama wapya.

## 3.4 UKOMO WA UWAKILISHI

Mwakilishi atakoma uwakilishi endapo.

(a) Atahama eneo lake la uwakilishi.
(b) Atakoma utumishi.
(c) Atajiuzuru mwenyewe.
(d) Kuisha kwa muda wa uwakilishi.
(e) Kifo.
(f) Atafukuzwa uanachama.
(g) Hachangii akiba ya lazima.

## 4.0 UCHAGUZI

Uchaguzi wa wawakilishi,wajumbe wa Bodi, kamati ya usimamizi, mwakilishi mkuu wa wanachama utafanyika kila baada ya miaka mitatu (3), na wanaostahili kuchaguliwa ni lazima wawe na utumishi usiopungua miaka mitatu kufikia kustaafu. Kwa mujibu wa sheria ya vyama vya ushirika No. 6 ya 2013 na kanuni zake za 2015, wawakilishi ni viongozi wa chama, watakaa kwa nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu (3) na wanaweza kuchaguliwa tena kwa miaka mingine mitatu, na si zaidi ya vipindi viwili mfululizo.

## 4.1 KAMATI YA UCHAGUZI

Kutakuwa na kamati huru ya kuratibu uchaguzi kama ilivyoainishwa katika kanuni ya 48 ya vyama vya Ushirika ya Mwaka 2015.

## 4.2 MCHAKATO WA KUWAPATA WAGOMBEA

### 4.2.1 DAFTARI LA WAOMBAJI

Kutakuwa na daftali la waombaji wa nafasi za uwakilishi litakalokuwa na kumbu kumbu zifuatazo:-

(a) Jina la mwombaji.
(b) Kikosi.
(c) Tarehe ya kuchukua fomu na muda.
(d) Tarehe ya kurejesha fomu na muda.
(e) Namba ya fomu.
(f) Namba ya uanachama.
(g) Tarehe ya kujiunga na chama.
(h) Namba ya simu ya mwombaji.

Ikiwa ni pamoja na taarifa zingine, kamati ya uchaguzi ikiona zinafaa kuongezwa ili kuleta ufanisi zaidi.

### 4.2.2 UPATIKANAJI WA FOMU

(a) Fomu za maombi zitapatikana kwenye kamandi, brigedi, vyuo, vikosi/viteule.

(b) Fomu zitakuwa na namba mwendelezo.

### 4.2.3 UJAZAJI FOMU

Kila mwombaji atachukua na kuijaza fomu kwa usahihi na kuirejesha makao makuu ya chama Mwenge – Mlalakuwa ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu kutangazwa tarehe ya kuchukua fomu kwa nafasi za uwakilishi.

## 5.0 TAREHE YA UCHAGUZI

Bodi itapanga tarehe ya kufanyika kwa uchaguzi siku arobaini na mbili (42) kabla ya mchakato mzima wa uchaguzi.

## 5.1 MUDA WA KUWASILISHA MALALAMIKO YA UCHAGUZI

Malalamiko ya uchaguzi yatawasilishwa kwa kamati ya uchaguzi ndani ya siku thelathini (30) baada ya matokeo ya uchaguzi.

## 5.2 NAFASI ZILIZOACHWA WAZI

Bodi ya chama baada ya kupokea taarifa ya nafasi zilizoachwa wazi, itapanga tarehe ya kufanyika uchaguzi ndani ya siku sitini (60), kuanzia tarehe ya kutolewa kwa taarifa. Taratibu zote za Uchaguzi wa wagombea zitafuatwa.

**HITIMISHO**

Sera hii imeandaliwa na Bodi ya Ngome SACCOS na Kamati ya Usimamizi iliyokasimiwa madaraka kwa niaba ya wanachama kwa barua yenye kumbukumbu Na. MA.82/309/20/14 ya tarehe 05 AGOSTI, 2020 na itaanza kutumika baada ya kuidhinishwa na Mrajis.

Mwenyekiti

NGOME SAVING AND CREDIT CO-OPERATIVE SOCIETY LIMITED
NGOME SACCOS LTD
REG. DSR 991
P.O. Box 35923
DAR ES SALAAM

Katibu

TANZANIA
Approved this 01ST
day of MARCH 2021
Asst. Registrar of Cooperative Societies